# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIKONGE**

**SIKONGE - TABORA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE.**

NAMBA YA USAJILI: S. 6411
SHULE YA SEKONDARI SIKONGE
S.L.P 181,
**SIKONGE-TABORA.**
TAREHE……………

**NAMBA ZA SIMU:**
MKUU WA SHULE: +255757260238
MAKAMU MKUU WA SHULE 1: +255 787 703 010
MAKAMU MKUU WA SHULE 2: +255 714956458
MLEZI WA WANAFUNZI: 0692674749

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi,

…………………………………

S.L.P………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SIKONGE ILIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE MKOA WA TABORA MWAKA...............................**

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka..................tahasusi ya ..........................................Shule ya sekondari Sikonge ipo umbali wa kilomita moja (01km) magharibi mwa makao makuu ya wilaya ya Sikonge karibu na Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Sikonge.

   Usafiri wa pikipiki /taxi/bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi Sikonge na nauli ni 2000/= kwa tax, pikipiki 1000/=, na bajaji 1000/=

   Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe………………..Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe… ......................na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe…………………

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1.** Sare ya shule

i. Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu na yasiyobana mwili
ii. Sketi mbili rangi ya kijani jeshi mshono wa linda box pana . urefu wa sketi ufike kwenye kifundo cha mguu. Kwa wavulana suruali mbili zenye rangi ya kijani jeshi [kitambaa kizito]
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi. Jozi mbili za soksi nyeupe kwa wasichana zisizo na mistari ya aina yoyote. Kwa wavulana soksi nyeusi .
iv. Wanafunzi wa kiislamu ; nusu kanzu nyeupe mbili kitambaa cha tetroni nzito na hijabu/juba nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua na zisizo na urembo wa aina yoyote.
v. Sweta la rangi ya kijani jeshi.
vi. Shamba dress wasichana gauni mbili za rangi ya maroon kwa ajili ya kushindia urefu ni mpaka kwenye kifundo cha mguu na mshono wa gauni ni solo. Wavulana suruali mbili rangi ya maroon
vii. T-sheti moja ya rangi ya kijivu.
viii. Tai moja rangi ya kijani jeshi.
ix. T-shirt ya kushindia moja rangi ya chungwa dhahabu kwa wavulana

NB: T-Shirt unaweza kuzipata Shuleni ukipenda.

**2.2. Mahitaji mengine MUHIMU ambayo mwanafunzi anatakiwa aje nayo shuleni.**

Mwanafunzi ajapo shuleni aje na :-

I. Kadi ya Bima ya Afya kama unayo njoo nayo na kama hauna utalazimika kuchangia fedha kiasi cha Shilingi 50,400/= (Ni lazima)
II. Madaftari ya kutosha Counter books Quire 3 [Idadi ni 07], penseli, kalamu, mathematical set(compass) na rula.
III. Vitabu vya tahasusi kulingana na tahasusi anayosoma kwa ajili ya kujisomea

binafsi.

IV. Mkanda wa kuvalia suruali ni wa ngozi mweusi wenye chuma moja.

V. Nguo za kulalia wavulana bukta rangi yoyote na wasichana night dress.

VI. Vitabu vya tahasusi yake. Orodha imeambatanishwa.

VII. Kikokotozi (scientific calculator).

VIII. Godoro futi 2.5x 6

IX. Mashuka pea mbili rangi ya pink ,blanketi moja , mto wa kulalia, foronya moja na chandarua moja.

X. Sanduku la bati (trunker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake

XI. Taulo moja (1), kwa wasichana vitenge au kanga doti moja, kwa matumizi binafsi.

XII. Tracksuit pea moja rangi ya kijani jeshi yenye mistari mieupe pembeni. Pamoja na jezi moja ya mikono mifupi rangi yakijani jeshi.

XIII. Raba za michezo jozi moja

XIV. Ndoo mbili ndogo zenye mfuniko

XV. Aje na vifaa vya usafi vifuatavyo :- fyekeo moja, ufagio wa ndani {soft broom 1}, ufagio wa nje (chelewa 1 zenye mipini mirefu na imara) (EGM), ufagio wa nje (chelewa 1 zenye mipini mirefu na imara), reki 1 isiwe ya kuchoma nondo (CBG), jembe lenye mpini 1 (CBG na EGM), brashi za chooni (za kusugulia masinki ya chooni 1 (CBG), Mopa/squezer 1 (EGBM))

## 2.3. michango ya shule

**a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :-**

| Na | MAHITAJI | KIASI (SH) |
|---|---|---|
| 1 | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000** |

Michango hii yote ilipwe kupitia **akaunti namba 51210024734** Jina la akaunti ni SIKONGE **SECONDARY SCHOOL-CAPITATION ACCT [NMB]**

***NB; HATUPOKEI FEDHA MKONONI MALIPO YOTE YAPITE BENKI*** **JINA LA MLIPAJI LIANDIKWE JINA LA MWANAFUNZI KWENYE PAY SLIP ZA BENKI KUEPUSHA USUMBUFU**

**b) Jumla ya michango yote ni Tsh. 80,000/=**

**3.O SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka I978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo :-

i. Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi na jamii yote kwa ujumla .
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli zifanyikazo shuleni.
iii. Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.
iv. Kufahamu na kuheshimu mipaka ya shule.
v. Kutotoka nje ya shule bila sare ya shule na ruhusa ya maandishi.
vi. Kutunza usafi binafsi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Ni marufuku kuwa bwenini wakati wa shughuli za darasani.
ix. Kuheshimu na kusimama wima bendera ya Taifa inapopandishwa au kushushwa na wimbo wa Taifa unapoimbwa.
x. Kuishi maisha ya ushirikiano na upendo na wenzako pamoja na jumuiya yote ya shule
xi. Kutotoa lugha ya matusi, kuzomea au kuanzisha fujo na kuanzisha au kushiriki katika migomo.
xii. Kusalimia wafanyakazi au mtu yeyote anayestahili anapopita ndani au nje ya darasa,
xiii. Kutomiliki kifaa chochote cha umeme kama vile pasi,chaja na simu.
xiv. Kulipa michango yote ya shule kwa wakati ili kuepuka usumbufu.
xv. Kufanya mitihani yote ya shule.
xvi. Kuvaa kitambulisho cha shule wakati wote ndani na nje ya shule.
xvii. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia shuleni zaidi ya saa 12 jioni.

## KUMBUKA;

1. Simu haziruhusiwi shuleni
2. Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani kwani atashindia sare za kushindia zilizoainishwa.
3. Mwanafunzi anaporipoti aje na fomu hii ikiwa na karatasi zote 11
4. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, kaka na dada na si mtu mwingine. Taarifa za msiba ziletwe moja kwa moja kwa mkuu wa shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.
5. Wageni wanaotambulika shuleni ni wale tu walioandikishwa kwenye faili la wanafunzi

na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula, mara mbili [2] kwa mwaka(kukiwa na ulazima wa kufanya hivyo.)

6. Likizo zote kwa mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwao.
7. Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia shuleni zaidi ya saa 12 jioni isipokuwa kwa dharura na taarifa kwa uongozi wa shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka.

**4.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZA KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi.
2. Uasherati , ushoga na Ubakaji.
3. Ulevi wa aina zote na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kuberi na kadhalika.
4. Kupigana au kupiga.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, binafsi au ya mwenzako.
6. Kudharau Bendera ya Taifa.
7. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kutoa mimba
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
10. Kufanya jaribio lolote la kujiua.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Kuwa na simu/laini ya simu ya mkononi shuleni.
13. Kutembelea majumba ya starehe na ya kulala wageni.
14. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.

Karibu sana katika shule hii

Helman Y. Mlembe

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SIKONGE
S.L.P. 181
SIKONGE

*FOMU NA.1*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**SIKONGE SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V Entrants.

Pupil's full name. ……………………………………………………………………

Age/Years ……………………………………Sex…………………………………

Blood found (red and white)……………………………………………………

Stool examination…………………………………………………………………

Urinalysis……………………………………………………………………………

Venereal Diseases test……………………………………………………………

T.B. Test: …………………………………………………………………………………

Eye Test.... ……………………………………………….'………………………

Ears……………………………………………………………………………………

Chest…………………………………………………………………………

Spleen…………………………………………………………

Abdomen……………………………………………………………………………

Urine for Pregnant……………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. Infections, chronic or family disease .

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: ……………………………..

Station……………………………………………..Date:…………………..

Official stamp……………………………………..

*FOMU NA.2*

**SHULE YA SEKONDARI SIKONGE**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………..
2. KABILA………………………………..
3. TAREHE Y A KUZALIWA … . . … .....MWEZI…. ......... MWAKA..................
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA ....................................................
5. MKOA WA………………………………………………..
6. DINI…………………………………………………DHEHEBU………………………
7. JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………...

(Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)

8. ANWANI YA MZAZI/MLEZI..................................................(KIJIJI)

…............................................... (TARAFA)

….......................................................(WILAYA)

…............................................................. (MKOA)

Na.za simu 1………………………………..

2………………………………………...

9. KAZI YA BABA/MLEZI……………………………………………………………
10. KAZI YA MAMA…………………................ ……………………………......
11. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari)
12. Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (majina matatu), anuani zao kamili na namba zao za simu
    a. Ndugu.....……………………………………………......Uhusiano……………..
       simu………………………………...
    b. Ndugu.....…………………………………………….......Uhusiano……………
       simu………………………………...
    c. Ndugu.....……………………………………………….....Uhusiano…………….
       simu……………………………………

……………………………        ……………………..

SAINI YA MWANAFUNZI        SAINI YAMZAZI/MLEZI

*FOMU NA.3*

**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi..........................................................................................................................(Jina kamili) ambaye ni mwanafunzi nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahala pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote .Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo, na
makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya
mwanafunzi……………………………
Tarehe………………………..

Shahidi
Jina
kamili……………………………………………..
Saini……………………..
Tarehe……………………..

*FOMU NA.4*

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi..................................................................................................................................(Jina kamili) ambaye ni

mzazi /mlezi wa. .............................................................................................................Kidato cha

............................... nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii na naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.
Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya

Mzazi/Mlezi……………………………

Anunani kamili…………………………………..

Tarehe…………………………

Simu………………………

# ORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAE KUJISOMEA YEYE BINAFSI

GEOGRAPHY

(i) Msabila D.T (2010). A comprehensive approach to physical geography

(ii) Msabila D.T (2010). Human geography for secondary schools

(iii) John M. Pritchard. Practical Geography for Africa

(iv) (R.B. Bunette), Physical Geography in Diagrams for Africa.

(v) Geography for Secondary Schools form five (TIE)

(vi) Human and Economical Geography by Gillan C. Morgan

vii)Msabila D.T (2010) Practical Geography for Secondary Schools

viii) Human and Economical Geography by Zisti Kamili

CHEMISTRY
i. ABC Chemistry For Higher Level
ii. Ramsed Chemistry For High Level And College

iii. Rodgers Muncaster For High Level And College

BIOLOGY
i. D.J. Taylor etal (1984): Biological Science 2nd or 3rd edition. Cambridge University press.uk
ii. Understanding Biology

ADVANCED MATHEMATICS REFERENCE BOOKS
1. Horril. P. J.F. ( 1985 ) , Pure Mathematics Book 2, 3rd Ed, Longman Group Limited, London.
2. Tranter . C. J. ( 1975) , ADVANCED LEVEL PURE MATHEMATICS, 4thEd,Hodder& Stoughton, London.
(VOLME II), S.CHAND & COMPANY LTD. New Delhi.
4. Hume. H. ( 1975 ) , An Introduction to Probability and Statistics, Revised Ed,University of Western Australia Press, Western Australia.

ECONOMICS
1.Economics Theory by Gupta
2.Micro-economics by Dwiverd
3.Economicsimplified By N A Saleemi
4.Modern Economics By Robert Mudida